WORKING TO EMPOWER

Ningezingatia Ushauri

Akaniambia itakuwa ni raha,
Alikuwa amekosea,
Kwa nini nilisikiliza?
Nilipaswa kukaa imara,
Na kusema la.

'Adero, tutakuwa salama bila kondomu, yeye akaniambia.
Kwa nini nilisikiliza?
Alikuwa amekosea.

Nilizihitaji zile fedha
Jamani ningefanya je?
Nimelipa gharama kubwa;
Ningezingatia Ushauri

Bila shaka haya yametendeka kwangu mbeleni,
Lakini nikawa mwenye bahati
Katika wakati huo.
Kapuuza ushauri
Wakati huu,
Na kuilipa gharama.

Mmoja wa asilimia sitini
ya maambukizi mapya
sasa mimi nimefanyika.
VVU / UKIMWI
Hiyo ndiyo iliyotokea.

Ningesikiliza,
Ningezingatia ushauri,
Lakini sikuwaza mara ya pili.

VCT - Ushauri na Upimaji wa Hiari
Mimi nilipuuza.
kaona haya, aibu
Kupata ushauri
Ijapokuwa mshauri alikuwa mwema.

Nimepata ugonjwa
Sasa ninao, naona haya na aibu
Kwa sababu sikusikiliza ushauri
Sikuwaza mara ya pili.

Adero anamgeukia rafiki wake wa dhati Akili kwa ushauri. Akili alipata kupitia hali sawia na hii, na amekuwa akipata baadhi ya masomo shuleni kuhusu afya ya uzazi na ushauri na upimaji (VCT).

Created by Sadia Ashraf, UK volunteer
Translated by Eric Nyaga, Kenya volunteer

Adero: Akili tayari wajua mamangu alikufa kutokana na UKIMWI. Bona nikawa mlegevu hivyo?

Akili: Rafiki yangu, wakati mwingine sisi huwa hatujapewa taarifa na msaada wa kutosha. Hili si kosa lako. Naweza kukusaidia sasa. Tunaweza kwenda kwa VCT na unaweza kupata ushauri na msaada. Wao watakupima kama una ugonjwa. Na unaweza kuzungumza na wasichana wengine vijana kama wewe. Utaona hauko peke yako.

Adero: Yeye aliniambia kondomu itasusha chini raha ya kimapenzi. Mimi hata sina uhakika kama nilitaka kufanya naye mapenzi.

Akili: Adero, kama huna uhakika unayo haki ya kusema la. Lakini walituambia shuleli ya kwamba kama umechagua kufanya mapenzi basi kutumia kondomu hafai kuwa ni kazi. Ninyi wawili mnaweza kusaidia kuivaa, na kufurahia wakati huu pamoja - hii inaongeza raha na uhusiano wa kimapenzi. Muhimu zaidi, ina waweka nyote wawili salama.

Adero: Kweli? Lakini nitaona haya kuzitumia kwani watu watafikiria mimi ni kahaba.

Akili: nilihisi hivyo pia. Lakini mwalimu aliniambia kwamba kama umeamua kufanya mapenzi kamwe usione aibu kuhusu kutumia kondomu au kuzungumza juu yake. Kutumia kondomu haimaanishi wewe ni kahaba. Alisema kwamba inafanya mapenzi kuwa salama nasi tunakaa tukiwa wenye afya.

Adero: Lakini Akili, si kutumia kondomu inamaanisha huna imani na mpenzi wako?

Akili: Kama mmoja wenu ana ukimwi basi kwa kutumia kondomu inaonyesha kuwa unamjali mpenzi wako kwani hutaki aambukizwe. Kutumia kondomu kunakuzuia kupata virusi vya UKIMWI. Mwalimu alituambia kwamba hata kama huna VVU / UKIMWI ni lazima utumie kondomu -hii ni tabia nzuri kwa shughuli zote za ngono. Kwa sababu sisi ni wanawake vijana vile mlango wetu wa uzazi unavyoendelea inamaanisha kuwa tumo katika hatari zaidi ya kupata magonjwa ya zinaa (STIs) pamoja na VVU, hivyo ni muhimu sana kwa afya zetu kutumia kondomu kila wakati.

Adero: Basi hatungefanya mapenzi.

Akili: Mwalimu alituambia kwamba hii ndio njia bora zaidi ya kukaa salama. Kama ni kusubiri bila kufanya mapenzi ... tusubiri hadi tuwe tayari. Na wakati tutakapokuwa tayari, tutumie kondomu.

Adero: Naam, ni mimi nimechelewa kwa wakati huu, lakini angalau kama nitamua kufanya mapenzi katika siku sijazo nitajua jinsi ya kukaa salama. Naona aibu kuuliza, lakini si kondomu sio zakutegemewa?

Akili: Ni sawa wala nisone aibu - tayari nimekwambia wewe. Mwalimu alituambia kwamba ni zakuaminika sana. alituambia kwamba kama umechagua kufanya mapenzi, tumia kondomu, na hutahitajika kuwa na wasiwasi kwa sababu utakuwa salama na kulinda kila mmoja kutokana na ugonjwa .. Kondomu ni nyembamba sana - huwezi kutambua tofauti.

Adero: Je, kama mpenzi wangu hataki kutumia kondomu?

Akili: pengine wao huwa na hofu kwa sababu hawajui habari za kutosha kuzihusu. Waambie yale niliyokuambia. Waambie kwamba itakuwa ni kuhakikisha nyote mko salama kimapenzi na hivyo nyote wawili mwaweza kutulia. Mwalimu pia alisema kama wewe una uzoefu katika kutumia kondomu mwambie mpenzi wako ni kwa nini wewe unapenda kuzitumia – mna aminiana; kuzungumza juu ya kondomu na kuzitumia ni njia nyingine ya kuonyesha imani yako.

Akili: Adero, somo lingine muhimu sana nililojifunza shuleli ni usalama wa kuwa na mpenzi mmoja. Tunavyo kuwa na wapenzi zaidi, ndivyo tunavyo weka afya yetu katika hatari. Mwalimu alituambia kwamba kama tutakaa na mpenzi mmoja mwaminifu tutakuwa na uhusiano wenye afya na wa kuaminika. Tutakuwa mifano mizuri kwa watoto wetu - hawatarudia makosa tuliyoyafanya.

Adero: (anacheka) Wewe unaishia maana ya jina lako, si ndio – mwenye busara sana. Asante kwa msaada wako wote Akili. Mimi kwa kweli nilijawa na hofu.

Created by Sadia Ashraf, UK volunteer
Translated by Eric Nyaga, Kenya volunteer

Akili: Ni sawa rafiki yangu. Mimi nilikuwa na hofu sana wakati yalifanyika kwangu. Nitakwenda na wewe kwa VCT - utaona kuna wengi kama wewe. Kuna msaada wako.

Adero: Lakini ni nini kitafanyika kwangu sasa? Niliona kile kilichotendeka kwa mamangu. Mimi nina hofu kuwa kitatendeka kwangu.

Akili: Tafadhali jaribu kutulia Adero. mama yako hakupata matibabu yoyote. Lakini wewe utapimwa. Mara tukijua hali yako kikamilifu basi unaweza kupata matibabu. Mwalimu alisema, kama una maambukizi ya VVU au UKIMWI basi kuna madawa unaweza kutumia. Hawawezi kutibu ugonjwa huo, lakini maisha yako yatakuwa bora zaidi kama utatumia madawa. Tutaweza kujua zaidi wakati tutakapo kwenda kwa mshauri.

Created by Sadia Ashraf, UK volunteer
Translated by Eric Nyaga, Kenya volunteer